# Uchanganuzi wa Mofu katika Kauli Mbalimbali za Mnyambuliko wa Vitenzi vya Silabi moja: Lahaja ya Ginantuzu

**Njana Masanja**
*Mwalimu Nyerere Memorial Academy, Tanzania*

***Uwasilishaji wa Makala***
Kupokelewa: 2025-01-28
Kurekebishwa: 2025-07-10
Kukubaliwa: 2025-07-14
Kuchapishwa: 2025-07-15

**Maneno Muhimu**
Ginantuzu
Kauli za vitenzi
Mfuatano
Mofu
Silabi

***Jinsi ya Kurejelea Makala:***
Masanja, N. (2025). Uchanganuzi wa Mofu katika Kauli Mbalimbali za Mnyambuliko wa Vitenzi vya Silabi moja: Lahaja ya Ginantuzu. *Journal of Kiswahili and Other African Languages, 3*(2), 19-29.

Copyright © 2025
CC BY NC SA

**Ikisiri**
Suala la mfuatano wa mofu katika kauli za vitenzi limewavuta wanaisimu wengi. Hata hivyo, hakuna utafiti ambao umefanyika katika Kisukuma lahaja ya Ginantuzu kuhusu mfuatano wa mofu katika kauli za vitenzi vya silabi moja. Kwa hiyo, makala hii ililenga kuchunguza uchanganuzi wa mofu katika kauli mbalimbali za mnyambuliko wa vitenzi vya silabi moja katika lahaja ya Ginantuzu. Lengo la makala hii lilikuwa kuchunguza vitenzi vyenye silabi moja na kubainisha mfuatano wa mofu katika kauli za vitenzi katika lahaja ya Ginantuzu. Utafiti ulifanyika katika kata za Sapiwi na Matongo wilaya ya Bariadi Vijijini. Vijiji viwili vilipitiwa na mtafiti. Vijiji hivyo ni Igegu na Matongo. Jumla wa watoataarifa 20 walifikiwa kwa uwiano sawa wa kijinsia. Vitenzi 80 viliteuliwa na mtafiti na kuwekwa katika kategoria mbili; vitenzi visoukomo katika kundi moja na vitenzi vya silabi moja katika kundi jingine na kupelekwa kwa watoataarifa. Watoataarifa waliteuliwa kwa kuzigatia kigezo cha usampulishaji lengwa. Data za makala zilikusanywa kwa mbinu ya Ushuhudiaji, mahojiano, hojaji na mapitio ya nyaraka za maktabani, makavazi na mitandaoni. Kama mwongozo wa kazi hii, makala imetumia nadharia ya Kanuni Tazamishi (KAT). Aidha, Mkabala wa kitaamuli ndio umetumiwa kubainisha mfuatano wa mofu na kauli. Matokeo ya makala ilibaini kauli sita (6) za vitenzi. Jumla ya vitenzi kumi vya silabi moja katika lahaja ya Ginantuzu vilipatikana. Makala pia imeonesha kuwa, baadhi ya vitenzi vya silabi moja havikubali kupokea baadhi ya mofu za kauli husika. Kikanuni, upangaji wa kauli hizi sio wa kubandika tu bali unafuata kanuni ya utokeaji wake.

## Utangulizi

Silabi ni neno au sehemu ya neno ambayo hutamkwa kwa pamoja kama fungu moja la sauti. Silabi inaweza kuundwa na irabu peke yake, konsonanti peke yake au konsonanti na irabu. Vitenzi vya silabi moja ni aina ya vitenzi ambavyo shina lake limejengwa na silabi moja (Waihiga 2010:147). Vitenzi vyenye silabi moja Mgullu (1999:116) alizielezea kama mofu funge kwa kusema kuwa "Mizizi ya vitenzi hivi ni mizizi ya mofu funge kwa sababu haviwezi kutumiwa peke yao kama neno na kuleta maana. Maana zao huwa hazijitokezi mpaka mizizi iwekewe viambishi. Vitenzi hivi huzalisha kauli mbalimbali, Kauli za vitenzi ni kategoria mojawapo katika ufafanuzi wa sentensi au kishazi ambayo hasa huhusu kitenzi (Massamba 2004). Kategoria hii hutumiwa kuonesha jinsi inavyoweza

kubadili uhusiano uliopo baina ya kiima na yambwa pasipo kubadilisha maana ya sentensi. Kwa kifupi kauli katika sarufi huhusisha uhusiano uliopo kati ya kitenzi, kiima na yambwa katika sentensi. Kauli za vitenzi vinaweza kuzalisha vitenzi vyenye kauli tofauti ili kuambanua tendo la mtu anayetenda. Kwa kawaida kitenzi kimoja kinaweza kudhihirisha hali tofauti kama vile hali ya kauli ya kutenda, kauli ya kutendea, kauli ya kutendana, kauli ya kutendwa, kauli ya kutendeka na kauli ya kutendesha na kauli ya kutendewa katika lugha mbalimbali duniani. Kwa mujibu wa Baraka (2018), mnyambuliko wa vitenzi ni jambo muhimu sana katika lugha zote. Maandishi mengi yanaonyesha kuwa kuna wasomi wengi sana ambao wameandika kuhusu mnyambuliko wa vitenzi katika lugha zote duniani. Kuna wasomi ambao wameandika kuhusu mnyambuliko wa vitenzi katika lugha ya Kiswahili na kuna wale ambao wameandika kuhusu mnyambuliko wa vitenzi katika lugha za Kibantu na zisizo za lugha ya Kibantu.

Kimsingi suala la mnyambuliko wa vitenzi ni mada ambayo imewavutia wanaisimu wengi duniani kote. Wanaisimu kama Khamisi (2008), Kiango (2008), Gawasike (2012), Mwita (2014) na Mbwillow (2017) walijikita kuchunguza mnyambuliko wa vitenzi katika lugha ya Kiswahili huku kila mmoja akichunguza vipengele kulingana na malengo ya utafiti wake. Watafiti wengine kama Mcpherson (2008), Asiimwe (2011), Charwi (2013) na Jepkoech (2018) walijikita katika kuchunguza mnyambuliko wa vitenzi vya Kiswahili/kibantu huku kila mmoja akimakinika na vipengele vyake kulingana na malengo ya utafiti wake.

Khamisi (2008) katika utafiti wake alichunguza jinsi unyambulishaji unavyoathiri kitenzi kisintaksia katika lugha ya Kiswahili. Matokeo ya utafiti wake yalionesha kuwa, unyambulishaji wenye mipaka huathiri tabia ya kitenzi kisintaksia kwa kuongeza yambwa, kupunguza yambwa au kutofanya chochote kile kwenye kitenzi. Pia katika utafiti wake alibaini kuwa, minyambuliko kama fanyizi, mufidi, ambatani, nafsi, tendwa, uwezo, tuamo na nyume hupelekea kitenzi kuteua kategoria za maneno.

Utafiti wa Khamisi (2008) umetoa mwongozo katika kazi yetu kwani, kazi yake imegusia kauli ya kutendesha na kutendwa ambao ndiyo dhana tuliyoshughulikia. Hata hivyo, utafiti huu ulijikita kuchunguza mfuatano wa mofu na kauli za vitenzi katika lahaja ya Ginantuzu ili kubaini mfuatano wa mofu, kauli na kanuni zinazotawala mfuatano huo ikilinganishwa na utafiti wa Khamisi (2008) uliojadili jinsi unyambulishaji unavyoathiri kitenzi kisintaksia katika lugha ya Kiswahili.

Kiango (2008) katika utafiti wake anasema kwamba, michakato yote ya unyambulishaji inatawaliwa na kanuni za kifonolojia na kimofolojia. Kanuni au michakato ya unyambulishaji wa vitenzi, zinatumiwa katika mizizi au mashina ya vitenzi kuzalisha aina mbalimbali za unyambuaji tenzi. Baadhi ya aina hizo ni kama vile unyambuzi- tendea, unyambuzi- tendana, unyambuzi- hali, unyambuzi-tendeshana unyambuzi-tendwa. Maelezo ya Kiango (keshatajwa) yalifaa katika utafiti huu kwani yamefafanua kanuni za kuzalisha vinyambuo-tenzi ambazo ndizo zilitumika katika kuchunguza mfuatano wa mofu na kauli za vitenzi katika vitenzi vya Kisukuma, lahaja ya Ginantuzu.

Gawasike (2012) alifanya utafiti kuhusu dhana ya uambikaji katika Kiswahili. Matokeo ya utafiti wake yalionesha kuwa, dhana ya uambikaji yana njia mbili ambazo ni uambishaji na unyambulishaji. Anafafanua dhana hizi na kutumia dhana ya uambikaji kwa kujadili uhusiano uliopo baina ya uambishaji na unyambulishaji. Anaendelea kusema kuwa uambikaji ni upachikaji wa mofu kabla na baada ya mzizi wa neno. Aidha, anasema kuwa uambikaji ni dhana ya juu ambayo imegawanyika katika sehemu mbili; uambishaji na unyambulishaji. Katika makala yake analenga kupendekeza matumizi ya uambikaji ili kutanzua utata ambao umekuwepo katika dhana

za uambishaji na unyambulishaji. Utafiti wa Gawasike (keshatajwa) umesaidia utafiti huu kwani amelishughulikia suala la uambikaji katika vitenzi ambapo anagundua kwamba ni upachikaji wa mofu baada ya mzizi ambapo watafiti wengine huiita unyambulishaji, na utafiti huu pia unahusu mfuatano wa mofu na kauli za vitenzi katika lahaja ya Ginantuzu ili kubaini mfuatano wa mofu, kauli na kanuni zinazotawala mfuatano huo.

Mwita (2014) katika utafiti wake alishughulikia dhima ya kiambishi cha kauli ya kutendea ya kitenzi cha Kiswahili. Katika kazi yake aliongozwa na kauli 'najivunia kuwa Mkenya' iliyojibiwa kwa kauli 'Navumilia kuwa Mkenya,' iliyokusudiwa kuzusha hisia za kizalendo. Mwita (keshatajwa) alilenga kuchunguza usarufi au utosarufi wa matumizi ya vitenzi "*najivunia*" na "*navumilia*" kwa mtazamo elezi na mtazamo elekezi. Katika utafiti wake Mwita (2014), alitambua kuwa kitenzi cha Kiswahili kina maumbo mbalimbali kama kauli ya kutendea. Maumbo haya ni kama vile {i}, {e}, {li}, na umbo {le} kutegemea na mzizi wa kitenzi. Makala ya Mwita (2014) pia ilizingatia dhima mbalimbali za kauli ya kutendea katika lugha ya Kiswahili.  Kazi ya Mwita (keshatajwa), ni tofauti kidogo na utafiti huu japo yeye alijikita tu kwenye kauli ya kutendea hasa kwa kushughulikia vitenzi viwili; ilhali utafiti huu unahusu mfuatano wa mofu na kauli za vitenzi vya silabi moja katika lahaja ya Ginantuzu ili kubaini mfuatano wa mofu, kauli na kanuni zinazotawala mfuatano huo.

Mbwillow (2017), akifafanua tofauti kati ya uambishaji na unyambulishaji katika Kiswahili, anaeleza kuwa maneno ya lugha asilia ya binadamu huundwa kwa njia mbalimbali. Anaeleza njia kama vile, uradidi, kubuni, uambatanishaji na uambatizi kwa maana ya uambishaji na unyambulishaji. Anaeleza kuwa uambikaji ni kitendo cha upachikaji au uongezaji wa mofu au viambishi kabla au baada ya mzizi wa neno, kiini au shina la neno. Anasisitiza kuwa njia kuu ya uundaji wa maneno iwe ni uambikaji kisha uambishaji na unyambulishaji ziwe ni aina ya uambikaji na tofauti yake kuu iwe ni pahala pa upachikaji. Katika kazi yake, anaeleza kuwa uambishaji na unyambulishaji huunda maneno mapya. Unyambulishaji hudokeza kauli mbalimbali. Anafafanua kauli ya kutenda, kutendewa, kutendeka na kutendeana. Anatoa mfano wa neno "lima" na kufafanua kama ifuatavyo; lim-i-a (kauli ya kutendea), lim-w-a (kauli ya kutendwa), lim-ik-a (kauli ya kutendeka) na lim-i-an-a (kauli ya kutendeana). Kazi ya Mbwillow (2017) ilitufaa katika utafiti huu kwani, alishughulikia suala la dhana ya kauli za vitenzi, dhana ambayo pia ilishughulikiwa katika utafiti huu. Hata hivyo, tofauti ya kazi yake na utafiti huu ni kuwa kazi yake ilihusu dhana ya uambikaji kama dhana kuu ilhali utafiti huu ulihusu mfuatano wa mofu na kauli za vitenzi vya silabi moja katika lahaja ya Ginantuzu ili kubaini mfuatano wa mofu, kauli na kanuni zinazotawala mfuatano huo.

Asiimwe (2011) alijadili mofimu za Utendea, Usababishi, Utendeka na Utendwa katika Runyankole, mojawapo ya lugha za Kiafrika. Matokeo ya utafiti wake yanaonesha kuwa, mofimu nyambulishi za usababishi hupokezwa kitenzi kwanza kabla ya utendwa. Anaeleza kuwa usababishi huunda kitenzi elekezi kutokana na kile ambacho sielekezi kwa sababu vitenzi elekezi tu ndivyo vinaweza kupokea utendwa. Utafiti wa Asiimwe (keshatajwa) ulitufaa katika utafiti wetu kwani utafiti wake ulihusika katika kauli zaa vitenzi. Hata hivyo, uafiti wake unatofautiana na huu kwani wake unahusu kauli tano za unyambulishaji wa vitenzi na utafiti wetu ulihusu mfuatano wa mofu na kauli za vitenzi vya silabi moja katika lahaja ya Ginantuzu.

Charwi (2013) alishughulikia unyambulishaji wa vitenzi katika Kikuria akiwa na lengo la kueleza matokeo ya vitenzi vya Kikuria baada ya unyambulishaji na idadi ya viambishi vinavyoweza kuwekwa pamoja kwenye kitenzi. Katika kazi yake, alichanganua unyambulishaji wa vitenzi ili kuonyesha dhana ya uelekezi unavyojitokeza na kuonyesha upekee na ufanano wa lugha ya Kikuria na lugha nyingine za Kibantu kama vile, Kinyambo, Kinyamwezi, Kibosho miongoni mwa lugha zingine. Utafiti wa Charwi (keshatajwa) ulilenga kufafanua athari za unyambulishaji kisintaksia.

Aidha, anagundua kuwa vitenzi vya Kikuria kama ilivyo kwenye lugha nyingi za Kibantu huwa na sifa tofauti tofauti kulingana na aina ya kitenzi. Kwa mfano, anasema kuwa vitenzi si elekezi havihitaji yambwa wakati vitenzi elekezi huhitaji yambwa moja au mbili kulingana na asili ya kitenzi chenyewe. Utafiti wa Charwi (2013) ulifaa utafiti huu kwani amegusia kauli mbalimbali za unyambulishaji wa vitenzi ambazo pia zimeshughulikiwa katika utafiti huu. Hata hivyo, utafiti wake unatofautiana na huu kwani alilenga kuonyesha athari za unyambulishaji kisintaksia hususan dhana ya uelekezi lakini utafiti huu ulichunguza mfuatano wa mofu na kauli za vitenzi vya silabi moja katika lahaja ya Ginantuzu.

Jepkoech (2018) alijadili mofimu ambishi na nyambulishi. Utafiti wake ulilenga kutambua ruwaza za upachikaji katika mpangilio wa vitenzi na kuchanganua kanuni za kimofosintaksia zinazoathiri upachikaji wa viambishi katika kitenzi cha Keiyo. Katika kazi yake, Jepkoech (keshatajwa) alitambua kwamba mofimu ambishi hutokea mwanzoni mwa kitenzi cha Keiyo isipokuwa zile ambazo huonyesha wakati uliopo na hali ya kuendelea. Alitambua pia kuwa mofimu nyambulishi hutokea mwishoni baada ya mzizi. Katika kazi yake, mtafiti alionyesha kuwa mofimu ambishi hufuata utaratibu wa wakati → ukanusho → hali → nafsi → mzizi. Kwa upande wa unyambulishaji alionyesha kuwa, mofimu nyambulishi huchukua taratibu mbalimbali. Utafiti wa Jepkoech (2018), ulitufaa katika utafiti wetu kwani ulishughulikia kauli za vitenzi sawa na utafiti huu japo utafiti wetu ulihusika tu na kauli za vitenzi vya silabi moja. Hata hivyo, kuna vitu vingi sana tumejifunza kuhusu kauli za vitenzi.

Ingawa kipengele cha Mnyambuliko wa Vitenzi kinaonekana kushughulikiwa na wanaisimu wengi kama walivyotajwa hapo juu, hakuna utafiti ambao umefanyika katika lugha ya Kisukuma, lahaja ya Ginantuzu kuhusu mfuatano wa mofu na kauli za vitenzi vya silabi moja. Kwa hiyo makala hii ililenga kuchunguza mfuatano wa mofu na kauli za vitenzi vya silabi moja katika vitenzi vya Kisukuma, lahaja ya Ginantuzu ili kuziba pengo.

Lengo la makala hii lilikuwa kuchunguza mfuatano wa mofu katika kauli mbalimbali za mnyambuliko wa vitenzi vya silabi moja katika lahaja ya Ginantuzu na kubainisha mofu na alomofu zinazopatikana katika mfuatano huo. Aidha, utafiti umechunguza vitenzi vya silabi moja na kubaini vitenzi kumi vya silabi moja katika lahaja ya Ginantuzu. Vitenzi saba vya silabi moja vya Ginantuzu vilinyambulishwa katika kauli za kutendea, kuendesha, kutendana, kutendeka, kutendwa na kutendewa.

## Kiunzi cha Nadharia

Makala hii ilitumia nadharia ya Kanuni Tazamishi (KAT) iliyoasisiwa na Baker (1985) na kufanyiwa marekebisho mwaka (1988) na (2002). Kimsingi, nadharia hii inaeleza kuwa, kuna uhusiano wa karibu kati ya mofolojia na sintaksia, yaani unyambulishaji kimofolojia lazima uakisi unyambulishaji wa kisintaksia. Kwa mujibu wa Baker (1993), sintaksia inatenda kazi katika sehemu mbili; mofimu na neno. Anafafanua zaidi kuwa maneno changamani huundwa na kanuni za kisintaksia hasa, mjongeo wa neno kuu kwa kugubika mzizi leksia katika mofimu. Mkabala huu unaeleza elementi zote zinazohusu mofolojia na sintaksia, maarufu kama Kanuni Tazamishi ya Baker (KAT) inayodai kuwa unyambulishaji kimofolojia unaakisi unyambulishaji sintaksia na kinyume chake. Ikiwa muundo wa kimofolojia wa neno changamani umetokana na mjongeo wa mzizi leksia katika maneno ambapo mofimu hizo zimeambikwa, KAT hufuatia moja kwa moja. Kama anavyodai Baker "mfuatano wa mofimu katika neno changamani unaakisi uambatizi asilia kisintaksia wa maneno ambayo yanashabihiana na mofimu hizo" (Baker  2002: 326).

Aidha, anadai kuwa KAT ni kanuni iliyoibuka ikihoji mtazamo wa sarufi zalishi uliojikita zaidi katika kuangalia dhima ya virai nomino na dhima za kidhamira na kupuuza vialamishi kimofolojia kama urejeshi, ambavyo vikiachwa tu vinaleta mvunjiko wa muundo wa sarufi. Pili, kikanuni, upo uwezekano mkubwa wa kuunda utendwa, kwa kuambika mofimu za utendwa katika nomino ambao ni sawa na uwezekano uliopo wa kuundwa umbo tendwa kwa kuambika mofimu tendwa katika vitenzi. Hivyo, haja ya kueleza kanuni ya uhusiano kati ya mofolojia na sintaksia iliyojidhihirisha katika fonolojia zalishi ilihitajiwa kuelezwa zaidi ya dhima zake. Lililo muhimu ni kuwa mofolojia inahusika na muundo wa neno, na sintaksia inahusika na muundo wa sentensi. Hata hivyo nyanja hizi mbili za kisarufi zinahusiana sana, wakati mwingine mpaka wake si wazi.

Baker, kwa kutumia KAT, anadai kuwa unyambulishaji sintaksia unaukilia mfuatano wa mofimu si tu katika lugha za Kibantu bali pia kiisimu kwa ujumla. Anafafanua zaidi kuwa; mpangilio wa kimofolojia hubainishwa na mfuatano wa mofimu ambao ni lazima ushabihiane na mfuatano wa mofimu kisintaksia wa lugha husika. Hii ina maana kuwa iwapo kitenzi kitapitia michakato miwili ya unyambulishaji kama vile, unyambulishaji tendea na tendana, mofimu tendea lazima zitokee karibu na mofimu mzizi kuliko mofimu tendana.

Manova na Aronoff (2010), wanabainisha sababu kuu mbili zinazosababisha hali hii ambazo ni utokeaji wa mofimu unaotawaliwa na kanuni, na utokeaji wa mofimu usiotawaliwa na kanuni.

Utokeaji wa mofu unaotawaliwa na kanuni unahusisha kanuni rasmi za kisarufi ambapo umbo na maana huzingatiwa zaidi. Umbo na maana vimejiegemeza zaidi katika masuala yahusuyo kanuni za kifonolojia, kanuni za kimofolojia, kanuni za kisintaksia na kanuni za kisemantiki.

Kwa mfano:

1. tabe-sase-rare-ta
   eat-CAUS-PASS-PAST
   'was made to eat'

Katika mfano hii kitenzi 'kula' kwanza kinapitia mchakato wa kauli ya kutendesha kisha kauli ya kutendwa. Aidha, mofu tendeshi zimetokea karibu na mzizi kuliko mofu tendwa. Katika mifano ya pili unyambulishaji tendea na unyambulishaji tendana ni kama ifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2. | a) pika | pikiana | pik-i- an-a |
| | b) soma | someana | som-e-an-a |
| | c) funga | fungiana | fung-i-an-a |
| | d) sema | semeana | sem-e-an-a |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 3. | a) zuga | gwiizugela | gwi-i-zug-el-a- | (pikiana) |
| | b) tola | gwiitolela | gwi-i tol-el-a | (oleana) |
| | c) soma | gwiisomela | gwi-i-som-el-a | (someana) |
| | d) seka | gwiisekela | gwi-i-sek-el-a | (chekeana) |

Mifano ya data hiyo kwa lugha zote mbili (a) Kiswahili na (b) Ginantuzu ni kuwa kimfuatano, mofu tendea huwa karibu kabla mzizi na kufuatiwa na mofu tendana baada ya mzizi. Hivyo katika kuwasilisha mfuatano wa mofimu nyambulishi wa vitenzi vya Ginantuzu tutatumia Kanuni Tazamishi (KAT) ya Baker (1985).

**Mbinu za Utafiti**

Makala hii ni matokeo ya utafiti wa kitaamuli kwa kiasi kikubwa na kitakwimu kidogo uliofanyikia maktabani na uwandani. Utafiti wa maktabani umetuongoza kupata kazi zinazohusiana na mada ambayo tumeshughulikia. Tumesoma vitabu, makala na kazi mbalimbali zinazotoa maelezo kuhusu mada husika. Data za makala hii zilikusanywa katika mkoa wa Simiyu katika wilaya ya Bariadi vijijini. Jumla ya kata mbili zilifanyiwa uchunguzi. Kata hizo ni Sapiwi na Matongo. Jumla ya vijiji viwili vilipitiwa na mtafiti ambavyo ni Igegu na Matongo. Sampuli ya watoataarifa ishirini (20) iliteuliwa na mtafiti kwa ajili ya mahojiano ili kukidhi lengo la makala. Wastani wa watu kumi (10) kwa kila kijiji walipatikana. Ili kupata sampuli hii, watoataarifa hao walisampulishwa kwa usampulishaji lengwa. Sampuli imechaguliwa kwa uhuru wa mtafiti ili kupata data iliyosaidia kufikia lengo la makala. Vitenzi ukomo na vitenzi visoukomo 80 viliteuliwa na mtafiti na kupelekwa kwa watoataarifa. Mtafiti katika nyakati tofautitofauti, alifanya mahojiano mbalimbali kuhusu vitenzi ukomo na vitenzi visoukomo. Uchambuzi na uwasilishwaji wa makala ulifanywa kwa njia ya kitaamuli. Kwa mujibu wa Walliman (2011), utafiti wa kitaamuli unajikita zaidi na uwasilishaji na uchambuzi wa data kwa kutoa ufafanuzi wake kimaelezo. Mkabala huu umekuwa faafu katika utafiti huu kwa kuwa tumetumia maelezo ya kiufafanuzi katika kubainisha mfuatano wa mofu katika kauli mbalimbali za mnyambuliko wa vitenzi vya silabi moja katika lahaja ya Ginantuzu.

**Matokeo ya Utafiti**

Matokeo ya makala ilibaini kauli sita (6) za vitenzi. Kauli hizo ni kauli ya kutendea, kauli ya kutendesha, kauli ya kutendana, kauli ya kutendeka, kauli ya kutendwa na kauli ya kutendewa. Jumla ya vitenzi kumi vya silabi moja katika lahaja ya Ginantuzu vilipatikana. Vitenzi hivyo ni:

| *Neno Kisukuma* | *maana Kiswahili* |
|---|---|
| a) cha | -fa (kufa) |
| b) lya | -la (kula) |
| c) nya | -nya (kunya) |
| d) ja | -enda (kwenda) |
| e) zwa | -vuja (kuvuja) |
| f) ng'wa | -nywa (kunywa) |
| g) swa | -tema (kutema kitu mdomoni) |
| h) pya | -ungua (kuungua) |
| i) gwa | -anguka (kuanguka) |
| j) zwa | -ota (kuota/chipuka kwa mmea) |

Makala pia imeonesha kuwa, baadhi ya vitenzi vya silabi moja havikubali kupokea baadhi ya mofu za kauli husika. Kikanuni, upangaji wa kauli hizi sio wa kubandika tu bali unafuata kanuni ya utokeaji wake.

**Kauli ya Tendea**

Kauli ya kutendea ni kitendo ambacho kinafanyika kwa manufaa ya, kwa niaba ya au kwa faida ya mtu au kitu kingine (Habwe, na Karanja 2004). Kauli hii huonesha kuwa nomino tenda ilitenda au inatenda au itatenda kitendo kwa niaba au kwa manufaa ya nomino tendewa. Katika makala hii, kauli ya kutendea kwa vitenzi vya silabi moja katika lahaja ya Ginantuzu inaoneshwa kwa alama //-

ele-// ambayo ni mofu ya kauli ya kutendea. Mifano ifuatayo katika 1 hapa chini inadhihirisha hali hiyo:

1.

| *Kauli ya kutenda Ginantuzu* | *maana Kiswahili* | *kauli ya tendea Ginantuzu* | *maana Kiswahili* |
|---|---|---|---|
| a) cha | -fa (kufa) | ch-el- a | fia |
| b) ja | -enda (kwenda) | j- el-a | endea |
| c) lya | -la (kula) | l-eel-a | lia |
| d) nya | -nya (kunya) | ny-eel-a | nyea |
| e) zwa | -vuja (kuvuja) | zw-eel-a | vujia |
| f) ng'wa | -nywa (kunywa) | ng'w-eel-a | nywea |
| g) swa | -tema (kutema) | sw-eel-a | temea |

Data hii, inaonesha kuwa mofu ya kauli ya kutendea kwa vitenzi vya silabi moja katika lahaja ya Ginantuzu ina alomofu mbili ambazo ni: //-el-// na //-eel-//. Alomofu //-el-// hutokea katika mazingira ambapo mzizi wa kitenzi cha silabi moja huishia na konsonanti kama katika (1) a na b, na alomofu //-eel-// hutokea katika mazingira ambapo mzizi wa kitenzi cha silabi moja unaishia na kiyeyusho *y* (c-d) na kiyeyusho *w* (e-g) kama katika (1) c, d, e, f na g.

**Kauli ya kutendesha**

Kauli ya kutendesha ni kitendo ambacho kinafanyika kwa kuonesha dhana ya usababisho kati ya nomino tenda na nomino tendwa/tendewa. Usababisho huu huweza kuwa ama mhusika fulani amesababisha kufanyika kwa kitendo na mhusika mwingine au mhusika mwingine amefanywa kutenda kitendo na mhusika fulani. Kauli ya kutendesha huonesha kuwa, umbo la kitenzi lioneshalo kuwa kiima ndicho kinachosababisha mtu au kitu kufanya au kuwa kitu. Katika makala hii, kauli ya kutendesha kwa vitenzi vya silabi moja katika lahaja ya Ginantuzu inaoneshwa kwa alama ya mofu //-ish-// ambayo ni mofu ya kauli ya kutendesha. Mifano ifuatayo katika 2 hapa chini inadhihirisha hali hiyo:

2.

| *Kauli ya kutenda Ginantuzu* | *maana Kiswahili* | *kauli ya kutendesha Ginantuzu* | *maana Kiswahili* |
|---|---|---|---|
| a) cha | -fa (kufa) | ch-ish- a | fisha |
| b) ja | -enda (kwenda) | j- ish-a | endesha |
| c) lya | -la (kula) | l-iish-a | lisha |
| d) nya | -nya (kunya) | ny-iish-a | nyesha |
| e) zwa | -vuja (kuvuja) | zw-iish-a | vujisha |
| f) ng'wa | -nywa (kunywa) | ng'w-iish-a | nywesha |
| g) swa | -tema (kutema) | sw-iish-a | temesha |

Data hii inaonesha kuwa mofu ya kauli ya kutendesha katika vitenzi vya silabi moja katika lahaja ya Ginantuzu ina alomofu mbili ambazo ni: //-ish-// na //-iish-//. Kanuni hii inafasiliwa kuwa alomofu //-ish-// hutokea katika mazingira ambapo mzizi wa kitenzi unaishia kwa konsonanti kama katika (2) a na b, na alomofu //-iish-// hutokea katika mazingira ambapo mzizi wa kitenzi cha silabi moja unaishia na kiyeyusho *y* (c-d) na kiyeyusho *w* (e-g) kama katika (1) c - g.

**Kauli ya kutendana**

Kauli ya kutendana ni kauli ambayo hubainisha uhusiano wa kufanyiana vitendo fulani baina ya nomino tenda na nomino tendwa. Katika kauli hii, nomino tenda na nomino tendwa huathirika na kitendo katika tungo. Upande mmoja unautenda upande fulani na upande huo unaotendwa nao unautenda ule upande mwingine. Hapa nomino zote katika tungo hufanya vitendo vinavyofanana

yaani mmoja anamtendea mwenzake kitendo hicho naye anatendewa hivyo hivyo. Dhana ya kauli ya kutendana inaweza kuelezwa kama kitenzi kinachohusisha pande mbili katika utendaji wa kiwango sawa (Ashton 1944). Katika makala hii, kauli ya kutendana kwa vitenzi vya silabi moja katika lahaja ya Ginantuzu inaoneshwa kwa alama //gwi-// ambayo ni mofu ya kauli ya kutendana. Mifano ifuatayo katika 3 hapa chini inadhihirisha hali hiyo:

3.

| *Kauli ya kutenda Ginantuzu* | *maana kiswahili* | *kauli ya kutendana Ginantuzu* | *maana Kiswahili* |
|---|---|---|---|
| a) cha | -fa (kufa) | *gwi-ch- a | *fana (kufana) |
| b) ja | -enda (kwenda) | *gwi-j-a | *endena |
| c) zwa | -vuja (kuvuja) | *gwi-zw-a | *vujana |
| d) lya | -la (kula) | gwi-ly-a | *lana (kulana) |
| e) nya | -nya (kunya) | gwi-ny-a | *nyana |
| f) ng'wa | -nywa (kunywa) | gwi-ng'w-a | *nyw-an-a |
| g) swa | -tema (kutema) | gwi-sw-a | temana |

**Muhimu:** *Alama ya* ***(*) kwa baadhi ya maneno inamaanisha vitenzi vya silabi moja ambavyo havikubali kupokea baadhi ya mofu za kauli husika.***

Data hii inaonesha kuwa mofu ya kauli ya kutendana katika vitenzi vya silabi moja katika lahaja ya Ginantuzu ina mofu moja ambayo ni //gwi-// yenye kumaanisha kutendana. Aidha, Kanuni hii inafasiliwa kuwa, baadhi ya vitenzi vya silabi moja vya Ginantuzu havikubali kupokea mofu za kauli ya kutendana kama katika (4) a – c). Vitenzi hivi kidhima vinaitwa **vitenzi si elekezi** ndio maana haviwezi kupokea mofu za kauli ya kutendana.

**Kauli ya Kutendeka**

Kauli ya kutendeka ni kauli ambayo haioneshi uhusiano baaina ya nomino tenda na nomino tendwa. Nomino tenda huathirika kutokana na kitendo husika. Kauli hii huelezea jambo ambalo limetendeka bila kutilia maanani watu waliotenda jambo hilo. Kitu kinachotiliwa maanani ni kule kutendeka kwa jambo fulani. Kauli hii hubainisha kuwa kitendo kimetendeka na kutimilika bila kuonesha aliyekitenda au kifaa kilichohusika katika utendaji wake. Kauli ya kutendeka ina sifa mbili. Mosi, kimofolojia kauli ya kutendeka hueleza jambo ambalo limetendeka, bila kutilia maanani watu waliotenda. Pili, kauli ya kutendeka huonesha uwezekano wa kitu kufanyika au kutokea. Katika makala hii, kauli ya kutendeka kwa vitenzi vya silabi moja katika lahaja ya Ginantuzu inaoneshwa kwa alama //gwii-// ambayo ni mofu ya kauli ya kutendeka. Mifano ifuatayo katika 4 hapa chini inadhihirisha hali hiyo:

4.

| *Kauli ya kutenda* | *maana* | *kauli ya kutendeka* | *maana* |
|---|---|---|---|
| a) cha | -fa (kufa) | *gwii-ch- a | *fika (kufika) |
| b) ja | -enda (kwenda) | *gwii-j-a | endeka |
| c) zwa | -vuja (kuvuja) | *gwii-zw-a | vujika |
| d) lya | -la (kula) | gwii-ly--a | lika (kulika) |
| e) nya | -nya (kunya) | gwii-ny-a | nyeka |
| f) ng'wa | -nywa (kunywa) | gwii-ng'w-a | nyweka |
| g) swa | -tema (kutema) | gwii-sw-a | temeka |

Data hii inaonesha kuwa mofu ya kauli ya kutendeka katika vitenzi vya silabi moja katika lahaja ya Ginantuzu ina mofu moja ambayo ni //gwii-//. Aidha, kanuni hii inafasiliwa kuwa, baadhi ya vitenzi vya silabi moja havikubali kupokea mofu za kauli ya kutendeka, kwa mfano katika (4) a - c.

Vitenzi hivi kidhima vinaitwa vitenzi si elekezi ndio maana haviwezi kupokea mofu za kauli ya kutendeka.

**Kauli ya Kutendwa**

Kauli ya kutendwa ni kauli ambayo hubainisha kuwa nomino tenda imetendwa au imetendewa jambo fulani yaani nomino tenda hupokea athari ya tendo. Ni kauli inayotumika kuwa mtu fulani au kitu fulani kimepokea tendo fulani. Kauli ya kutendwa huonesha kuwa katika kitenzi husika kiima kina uamilifu/dhima ya kutendwa; yaani kinafanyiwa tendo (Ashton 1944). Aidha, Mkude (2005:119) kwa kuzingatia dhima za kidhamira ya data alizozifafanua katika Kiswahili anadai kuwa, kimofolojia utendwa umegawanyika katika aina kuu nne ambazo ni: utendwa tenda, utendwa pokezi/lengo, utendwa mhisi na utendwa uso-binadamu. Hata hivyo katika makala hii, hatushughuliki na aina hizo nne za kauli za kutendwa, kwani sio kusudio la makala hii. Katika makala hii, kauli ya kutendwa kwa vitenzi vya silabi moja katika lahaja ya Ginantuzu inaoneshwa kwa alama ya mofu //-iw-// ambayo ni mofu ya kauli ya kutendwa. Mifano ifuatayo katika 5 hapa chini inadhihirisha hali hiyo:

| 5. ***Kauli ya kutenda Ginantuzu*** | ***maana Kiswahili*** | ***kauli ya kutendwa Ginantuzu*** | ***maana Kiswahili*** |
|---|---|---|---|
| a) cha | -fa (kufa) | *ch-iw- a | *fiwa (kufika) |
| b) ja | -enda (kwenda) | * j-iw-a | *endwa |
| c) zwa | -vuja (kuvuja) | *zw-iw-a | vujwa |
| d) lya | -la (kula) | ly-iw-a | *lwa (kulika) |
| e) nya | -nya (kunya) | ny-iw-a | *nywa |
| f) ng'wa | -nywa (kunywa) | ng'w-iw-a | *nywwa |
| g) swa | -tema (kutema) | sw-iw-a | temwa |

Data hii inaonesha kuwa mofu ya kauli ya kutendwa katika vitenzi vya silabi moja katika lahaja ya Ginantuzu ina alomofu moja ambayo ni: //-iw-//. Aidha, kanuni hii inafasiliwa kuwa, baadhi ya vitenzi vya silabi moja havikubali kupokea mofu za kauli ya kutendwa, kwa mfano katika (5) a - c.

Vitenzi hivi kidhima vinaitwa **vitenzi si elekezi** ndio maana haviwezi kupokea mofu za kauli ya kutendwa.

**Kauli ya Kutendewa**

Kauli ya kutendewa ni kauli ambayo hubainisha kuwa nomino tenda inenufaika au imepata hasara ya tendo lililofanyika. Ni kauli inayotumika kuwa yupo mtu au wafu wanaotenda jambo fulani kwa niaba ya mtu au watu wengine. Tunaweza kusema kuwa wanaotendewa ndio wanaonufaika au wanaopata hasara. Katika makala hii, kauli ya kutendewa kwa vitenzi vya silabi moja katika lahaja ya Ginantuzu inaoneshwa kwa alama ya mofu //-elw-// ambayo ni mofu ya kauli ya kutendewa. Mifano ifuatayo katika 6 hapa chini inadhihirisha hali hiyo:

6.

| ***Kauli ya kutenda Ginantuzu*** | ***maana Kiswahili*** | ***kauli ya kutendewa Ginantuzu*** | ***maana Kiswahili*** |
|---|---|---|---|
| a) cha | -fa (kufa) | ch-elw- a | fia (kufiwa) |
| d) ja | -enda (kwenda) | j-elw-a | endewa |
| e) zwa | -vuja (kuvuja) | zw-elw-a | vujiwa |
| b) lya | -la (kula) | l-elw-a | *liwa (kuliwa) |
| c) nya | -nya (kunya) | ny-elw-a | nyewa |
| f) ng'wa | -nywa (kunwa) | ng'w-elw-a | *nywewa |
| g) swa | -tema (kutema) | sw-elw-a | temewa |

Data hii inaonesha kuwa mofu ya kauli ya kutendewa katika vitenzi vya silabi moja katika lahaja ya Ginantuzu ina mofu moja ambayo ni //-elw-//. Aidha, kanuni hii inafasiliwa kuwa, vitenzi vyote vya silabi moja vya Ginantuzu katika kauli ya kutendewa vinakubali kupokea mofu za kauli ya kutendewa, kwa mfano katika (6) a - g.

**Hitimisho**

Kauli za vitenzi vya silabi moja katika lahaja ya Ginantuzu vimeonesha kuwa na jumla ya vitenzi kumi (10). Kauli hizo pia vimeonesha kuwa, baadhi ya vitenzi havikubali kupokea baadhi ya mofu za kauli ya husika. Upangaji wa kauli hizi unafuata kanuni ya utokeaji wake. Kwa mfano, kauli ya kutendwa ili itokee sharti itanguliwe na kauli nyingine ambazo ni ama kauli ya kutendesha au kauli ya kutendea. Hali hii husababishwa na mchakato mmoja kutokea kwanza na kuukilia utokeaji wa mchakato mwingine. Yaani neno linaloundwa kwanza baada ya kunyambulishwa hatua ya kwanza, mzizi nyambulishi unadhibiti mofu nyambulishi zitakazokuja baada ya zenyewe.

Mwisho, tunapendekeza uchunguzi zaidi wa kiisimu juu ya vitenzi vya kisukuma na lugha zingine za kibantu ili kulinda, kuhifadhi na kuendeleza takwimu za kiisimu juu ya lugha za kibantu na zisizo za kibantu kwa manufaa ya kizazi kijacho.

**Marejeo**

Ashton E. O. (1944). *Swahili Grammar: Including Intonation*. Longman Group Ltd.

Asiimwe, C. (2011). *Unyambulishaji wa Vitenzi katika Lugha ya Runyankole*. Tasnifu ya Uzamili. (haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Baker, M. (1985). The Mirror Principle and Morphosyntatic Explanation, *Linguistics Enquiry* 16: 373 – 415.

Baker, M. (1993). Noun incorporation and the nature of linguistic representation. *The role of theory in language description*, 13-44.

Baker, M (2002). "Building and Merging, not Checking: the nonexistence of (Aux)-SVO language" *Linguistics Enquiry* 33: 321- 328.

Baraka, Y. (2018). *Unyambulishaji wa Vitenzi vya Lugha ya Kinyakyusakatika Mkoa wa Mbeya Kyela*. Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino.

Charwi, Z. M. (2013). Unyambulishaji na Dhana ya Uelekezi katika Lugha ya Kikuria, katika Omari, S. na Peterson, R. (wah). *Kioo cha Lugha*, 11, (uk 58-77). Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

Gawasike, A. (2012). *Dhana ya Uambikaji katika Kiswahili*. Tasnifu ya Uzamili. (haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Habwe, J., & Karanja, P. (2004), *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili.* Phoenix Publishers.

Jepkoech, N. S. (2018). *The Morphosyntax of the Keiyo Verb*. (Unpublished M.A. Thesis). Moi University.

Khamisi, A. M. (2008). *Maendeleo ya Uhusika*. TUKI.

Kiango, J. G. (2008). Sarufi ya Vinyambuo Vitenzi vya Kiswahili: Mitazamo Mbalimbali kuhusu Kanuni za Unyambuaji, katika Ogechi, O. N. Shitemi, N., Manova, S. and Mark, A. (2010), "Modeling affix order in Affix Combinations1", *Special issues of Morphology*, Manova, Aronoff (eds).

Manova, S. & Mark, A. (2010), "Modelling affix order in Affix Combinations1", *Special issues of Morphology*, Manova, Aronoff (eds). DOL: 10.1007/S11525-010-9153-6.

Massamba, D. (2004). *Sarufi misingi ya sarufi ya Kiswahili*. Phoenix Publishers.

Mbwillow, S. N. (2017). *Uambikaji kama Dhana Kuu: Tofauti ya Uambikaji na Unyambulishaji*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

McPherson, L. (2008), *A Descriptive and Theoretical Account of Luganda Verbal Morphology*, Unpublished Bachelor Dissertation, Srips College.

Mgullu, R. S. (1999), *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili.* Longhorn Publishers.

Mkude, D. J. (2005), *The Passive Construction in Swahili.* Tokyo, Research Institute for Languages and Cultures of Asia and Africa (ILCAA).

Munene, A. S. (2011). *Uanishaji wa Mofimu za Kisarufi katika Kitenzi cha Kichuka*. Tasnifu ya Uzamili (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Chuka.

Mwita, L. C. (2014). Najivunia kuwa Mkenya: Utosarufi, Mtindo au Mabadiliko ya Lugha? Katika Simala, I., Chacha, L. & Osore, M. (wah). *Miaka Hamsini ya Kiswahili Nchini Kenya* (uk 179-187) Twaweza communications.

Waihiga, G. (2010), *Sarufi Fafanuzi ya Kiswahili.* Longhorn Publishers.

Walliman, N. (2011). *Research Methods: The Basic.* Routledge.